ECHO East Africa

(Regional Impact Center)

Newsletter

Aprili 2014 **Jarida la 003**

Salaam kutoka ECHO kituo cha Afrika Mashariki!

Katika makala haya:

1. Kongamano la wakulima wafugaji
2. Ziara ya Burundi
3. Benki ya Mbegu ECHO
4. Matunda:"Banana Passion Fruit"
5. Viazi vitamu vya lishe
6. Mada za kutafakari

Kalenda ya matukio mbalimbali:

Permaculture Design Course
Presented by FoodWaterShelter
May 26th – June 6th
English and Kiswahili!
Details Here!

NaneNane 2014
Agricultural show in Njiro
August 1st – August 8th
Details Here!

ECHO East Africa Highlands Symposium
October 28th – 30th2014
Mark Your Calendars Now!
Details Here!

Kongamano Wafugaji liloandaliwa na ECHO kituo cha Afrika Mashariki

Katika wiki ya kwanza ya mwezi machi, zaidi ya washiriki 125 kutoka nchi mbalimbali, walikusanyika Machakos, Kenya kuzungumzia mbinu bora mbalimbali za jinsi ya kumuinua mfugaji. Mada mbalimbali ziliweza kuzungumzwa kwa washiriki wote wakati wa asubuhi na kugawanyika katika vikundi vya mada mahususi wakati wa jioni kwa muda wa siku tatu.Siku ya nne ilikuwa ni ya hiari ya washiriki kwenda kutembelea malambo ya maji ya mchanga (sand dams).
Mada zilizowasilishwa ni pamoja na zifuatazo:

- Kurejesha urithi wa misitu kwa kutumia njia ya visiki hai (Farmer Managed Natural Regeneration, FMNR) tazama picha hapo juu.
- Kuboresha Afya za mifugo kwa kutumia mbinu mbalimbali endelevu (Sustainable practices and health of livestock)
- Program shirikishi za chanjo ya wanyama kwa kutumia wahudumu jamii. (Animal immunization programs and community animal health workers)
- Kilimo mseto cha hifadhi ya ardhi na ufugaji (Integration of pastoralism and conservation)
- Kilimo Hifadhi (Conservation Agriculture,CA)
- Njia bora mbalimbali za uchujaji wa maji salama na utunzaji (Various water storage methods and purification techniques)
- Jinsi ya kuendeleza amani katika jamii za kifugaji (Peace making among people and livestock)
- Kilimo hifadhi kwa njia Mungu anavyofurahia -Farming God's Way

Unapata shida kujiunga na tovuti yetu ya ECHO? Jifunze zaidi kwa kubofya: Check out our basic tutorial here.

Mtambue: Brian Lawrence

Mnamo mwezi wa Februari 2014, ECHO Afrika ya Mashariki ilipata mtaalamu wake wa pili kutoka ECHO Florida. Brian amesoma Biolojia katika chuo cha Hanover College - Indiana, USA kabla ya kujiunga na ECHO mwaka 2012. Amekaimu kama meneja wa benki ya mbegu ECHO Florida mwaka 2013 na baadae kuja ECHO Afrika Mashariki ambapo anashiriki kuanzisha na kujenga benki ya mbegu ya kituo, pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na kushiriki kazi za kila siku. Mawasiliano yake ni: blawrence@echonet.org

ECHO inamshukuru kila mtu ambaye alihudhuria kongamano hili. Tunatarajia kuwa na matukio kama haya katika siku zijazo! Kama una picha au hadithi kutoka kwa tukio hili, tafadhali tushirikishe ekinsey@echonet.org au www.echocommunity.org!

Machapisho mbalimbali ya kongamano hili yanapatikana SASA!!

Wakati na baada ya kongamano, tumeweza kuweka kwenye mtandao wa intaneti machapisho mbalimbali ambayo unaweza kuyapata kwa kubofya mtandao wetu wa www.ECHOcommunity.org Hata kama hukuhudhuria kongamano la ECHO unakaribishwa kuangalia machapisho mbalimbali kupitia 2014 Pastoralist Symposium Presentations.

Unasisitizwa kujiunga kuwa mwanachama kama bado hujasajailiwa na ECHOcommunity ili kupata machapisho na majarida mbalimbali Kujiunga BONYEZA HAPA: CLICK HERE

Ziara ya Burundi:

Mkurugenzi wa ECHO kanda ya Afrika Mashariki, alifanya ziara ya ya wiki moja mafunzo yaliyodhaminiwa na FIDA International. (kuanzia Aprili 6 hadi 13). Mafunzo ya siku tatu yalifanyika kwa wachungaji ishirini na saba wa makanisa ya Burundi (Burundi's Pentecostal Church of Burundi – CEPBU's) kutoka katika majimbo 15 ya nchi hiyo. Mafunzo yalihusu mada za usalama wa chakula na mabadiliko ya tabia nchi (food security & climate change, environment management & protection), kilimo hifadhi (conservation agriculture – CA) na upandaji wa miti (tree planting). Wakati wa uwasilishaji; lugha tatu za kiingereza, kiswahili na kirundi zilitumika, ili kuwawezesha wachungaji waelewe vyema na hivyo kwenda kufundisha katika jamii walizotokea.

Picha za hapo juu kuanzia kushoto kufuatia mzunguko wa saa: jamii wakiwa eneo la soko karibu na barabara kuu, na kulia ni nyanda za juu za Burundi zinavyoenekana wakati watoto wanaotumika wakati mwingine kwa kazi nzito kama kubeba mizigo

Baada ya mafunzo, kulikuwepo na ziara ya siku mbili iliyoratibiwa na wadau pamoja na makanisa ya CEPBU.Jamii mbili za waliokuwa wakimbizi kutoka Tanzania na jamii zenye ulemavu ziliweza kutembelewa. Jamii za waliokuwa wakimbizi zilizotembelewa ni pamoja na Rutana, Giharo na kanisa la Bukemba. Kanisa la

Mkurugenzi wa ECHO Afrika ya Mashariki ameungana na wandaaji wa chapisho jipya la FAO kama mmoja wa wahariri ambalo unaweza kulisoma kwenye mtandao: Decision Tools for Family Poultry

CEPBU vilevile linaendesha kituo cha walemavu cha Gakwende kinachomilikiwa na kanisa la Kiremba; na vilevile CEPBU wanaendesha kituo cha kilimo cha ItabMweya Agriculture Technical School kilichopo mkoa wa Gitega, na kusaidia kanisa la Gitega (Gitega Pentecostal Church).

Mkurugenzi wa ECHO alipata fursa ya kuongelea uwezekano wa kufanyika kwa kongamano la kilimo endelevu katika nyanda za juu nchini Burundi kati ya mwaka huu 2014 au ujao 2015. Kulikuwepo na maelewano chanya na hivyo wadau kukubaliana pamoja na uongozi wa ECHO, na maridhiano yakawepo kongamano hilo kufanyika mwaka huu mwezi wa kumi kuanzia tarehe za 28 hadi 30 Oktoba mjini Bujumbura-Burundi. Angalia https://echocommunity.site-ym.com/?EAHighSymposium2014

Picha juu: Mkurugenzi wa ECHO (kushoto) katika picha ya pamoja na washiriki wengine nchini Burundi.

Ujenzi wa benki ya mbegu katika kituo cha ECHO kanda ya Afrika Mashariki.

Kituo cha ECHO kanda ya Afrika Masharika kinahitaji kujua aina ya mbegu unazofikiri ni vema zikapatikana katika kanda yetu.Tushauri kwa kubonyeza : HAPA

Kituo cha ECHO kanda ya Afrika Mashariki kinajivuna kuwatangazia uanzishwaji wa benki ya mbegu katika ukanda huu! Ujenzi wa chumba baridi (cold room) kwa ajili ya utunzaji wa mbegu kwa muda mrefu, ulianza mwezi Machi 2014 sambamba na zoezi la ukusanyaji wa mbegu mbalimbali. Kituo cha ECHO kimefanikiwa vilevile kununua mashine ya kupunguza hewa kwenye vifaa na kontena zinazohifadhia mbegu ijulikanayo kama 'vacuum packing machine' ili kuboresha uhifadhi na umri wa mbegu. Benki ya kanda ya mbegu inaweza kukusanya mbegu kutoka katika vyanzo mbalimbali kama, mbegu za kienyeji,mbegu za mazao ya chakula, matunda, mbogamboga, viungo nk., na vilevile kupata mbegu kutoka kwenye mabenki mengine ya mbegu ulimwenguni kwa kupanua wigo wa kimtandao.Ni matumaini makubwa ya ECHO kwamba benki hii ya mbegu itasaidia wakulima wadodo wadogo kupata mbegu za majaribio ya mazao funika (green manure or cover crops - GM/CC's),mbegu za kienyeji,mbegu zenye kustahimili mazingira tofauti yaliyo magumu,na mbegu za matunda na mboga za asili ambazo zipo kwenye mashaka makubwa ya kupotea kutokana na kutolimwa na kuzalishwa. Taratibu na itifaki za jinsi ya kushirikishana utoaji wa mbegu katika kanda ya Afrika Mashariki utazingatiwa ili kukidhi mahitaji ya wanachama na wadau kupata mbegu zilizotajwa hapo juu katika benki hii.

Jinsi gani utakavyohusika? ECHO inategemea wahisani na wamisionari wa Afrika Mashariki na wadau wengine wa maendeleo kukusanya na kugawana mbegu mbalimbali ambazo unahitaji kujaribu kuzipanda.Kama zilivyo benki nyingine za mbegu za ECHO ikiwa ni pamoja na ya nchini Thailand, na ile ya kimataifa iliyopo Florida, Marekani. Hata hivyo ECHO inaendelea kuwashauri wanamtandao wake kutumia mbegu za asili walizonazo zaidi ya kutegemea zitakazotolewa na ECHO. Vilevile ECHO inahamasisha na kuwashauri wadau mbalimbali kukusanya na kuleta mbegu nzuri katika vituo vya ECHO ili zihifadhiwe na hata kuzizalisha zaidi. Mbegu

hizi budi ziwe zenye afya nzuri,zisizo na magonjwa wala wadudu, na zenye taarifa ya kumbukumbu za historia yake, na ubora wake katika eneo mbegu inakotoka.Tungefurahi kujua kuhusu historia ya mbegu uliyonayo kwa kushirikiana nasi kwa kupitia Seed Forum na vilevile tungependa ushauri wako kuhusu tazamio letu la kuwa na benki ya mbegu ya ECHO kanda ya Afrika Mashariki kwa kupitia: Recommend Seeds Here

---

Jaribu mbegu hizi:Banana Passionfruit

Matunda yajulikano kama "*banana passion fruit*" (kama yanavyoonekana katika picha hapa chini) ni matunda nadra katika jamii yetu ambayo kituo cha ECHO kanda ya Afrika Mashariki imeyapata kutoka Kenya. Kwa jina la kitaalamu yanajulikana kama "*Passiflora tarminiana"*.Matunda haya yamechimbukia Kusini mwa Marekani na mara nyingi yanapandwa kama mapambo zaidi ya matunda. Kama jamii ya mapasheni yalivyo, matunda haya huota kwa kutambaa. Matunda haya yamekaa muundo kama wa ndizi ndogo ndogo zilizonyooka kama ilivyo jina lake na yana rangi mchanganyiko wa zamabarau na nyekundu. Matunda haya yanaweza kuliwa mara baada ya kuvunwa yakisha wiva, au yakatengenezewa juisi au kama matunda ya mezani baada ya mlo.

- Je unajua kuwa matunda haya yanaustahimili wa baridi na yanaweza kutumika kama miche mama kwa ajili ya kuzalishia matunda mengine jamii ya mapasheni?

Pichani juu: Matunda yaliyoiva ya *"banana passion fruits"* yakiwa yamevunwa kwa ajili ya mbegu (zinazoonekana picha ya kulia).

Kama unahitaji mbegu hizi, tafadhali fika katika ofisi yetu ya ECHO Kanda ya Afrika Mashariki. Tafadhali fuata maelekezo haya hapa Directions to the ECHO East Africa Center ya ya jinsi ya kufika ofisini kwetu.

Je unazo mbegu ambazo ni za ziada kwako na ungependa kugawanya na wadau wengine kupitia kituo cha ECHO Kanda ya Afrika Mashariki ofisi za Arusha? Mbegu hizi zitawasaidia na wengine katika kanda hii ya Afrika Mashariki. Tafadhali wasiliana nasi kupitia kwa: blawrence@echonet.org au ekinsey@echonet.org

---

Mbegu za viazi vitamu lishe zinapatikana

Viazi vitamu (*Ipomoea batatas*) ni miongoni mwa mazao saba bora ya chakula duniani, vikifuatiwa na ngano, mchele, mahindi, viazi, shayiri na mihogo. Kutokana na maandishi mbalimbali mfano Franklin Martin wa ECHO anaandika kwamba, Viazi Vitamu Lishe – Orange Fleshed Sweet potato (OFSP) vina vitamini A kwa wingi muhimu kwa watoto wenye utapia mlo hasa kusini mwa jangwa la Sahara. (Franklin Martin, ECHO Technical Note) Madhara ya ukosefu wa vitamini A ni pamoja na kusababisha upofu, kudumaa kwa akili, hupunguza kinga ya mwili na husababisha magonjwa kama kuharisha, surua na magonjwa mengine.

Katika mwezi wa Novemba 2013, mwanzilishi kiongozi wa ECO Agri Consult (tazama: EcoAgriConsult) Bwana Wilfred Mushobozi , alialika watumishi wa ECHO katika mafunzo bora ya kilimo cha viazi vitamu lishe, yaliyohusu hatua kuu nne za uzalishaji wa mbegu kuanzia maabara (Tissue Culture) hadi kwa mkulima – mzalishaji. Kituo chake kinazalisha miche mbalimbali kwa njia ya vipandikizi vya "*tissue culture"* kwenye mimea mbalimbali ikiwa ni pamoja na migomba ya aina mbalimbali.mihogo, kahawa pamoja na viazi vitamu hasa katika hatua kuu mbili za awali kabla ya usambazaji kwa wakulima. Katika hatua ya pili ya kuzalisha mbegu za viazi vitamu, ECHO iliweza kukuza zaidi ya miche mia sita (600) katika hatua ya pili ya usambazaji mbegu na kuweza kupata mbegu bora za kupanda hatua ya tatu kwa ajili kuuza na yakugawia wakulima kwa hatua ya nne ya kupanda katika mashamba yao. Mfumo huu wa uzalishaji una lengo la kuboresha mifumo ya usambazaji ili kufikia wateja wengi zaidi na washirika mbalimbali wanaohasimiana na ECHO

Pichani juu: Adiveckson Harold anaonyesha mbegu bora za viazi vitamu katika hatua ya tatu (3) katika kituo cha ECHO.

Juhudi za uzalishaji huu wa mbegu umekubalika sana na wakulima na vilevile kukubaliwa na baadhi ya wadau wa maendeleo kama vile Dr Francis Shao ambaye alimwalika mfanyakazi wa ECHO (Adiveckson Harold, anayesimamia bustani ya ECHO) kumsaidia katika kuanzisha vitalu viwili vya miche yenye idadi ya miche mia tatu (300) kila kimoja cha miche bora ya viazi vitamu lishe (OFSP) yapata umbali wa kilomita 140km kutoka ofisi ya ECHO . Lengo la mdau huyu ni kuwaelimisha vijana hasa wa shule za msingi kuelewa stadi za maisha maisha na jinsi ya kujitegemea kupitia kilimo endelevu na kuboresha lishe zao nyumbani. Juhudi hizi vilevile ziliweza kutambuliwa na mfanyakazi mratibu wa shirika lisilo la kiserekali la FIDA – Eastern Africa Regional Food Security and Climate Change Project; bwana Lomayani Laizer ambaye alibainisha kuwa ECHO wamekuwa wabunifu wa kutatua

tatizo la umaskini miongoni mwa watu wa maeneno yanayozunguka kituo kwa kutumia mbinu mbalimbali bora za kilimo na lishe bora.

Katika msimu huu wa mvua, ECHO kwa kushirikiana na EcoAgriConsult imesaidia kutoa mafunzo na utoaji wa vipandikizi visivyopungua 20 vya viazi vitamu lishe (OFSP) kwa kila mkulima aliyehudhuria mafunzo.

Wakulima wengine walioalikwa na ECHO kuangalia na kujifunza zaidi kuhusu viazi vitamu lishe (OFSP).
Hivi sasa ECHO inaendelea kushirikiana na wadau wengine katika kuhimiza usambazaji wa mbegu za viazi vitamu lishe (OFSP) aina za *'Kabode'* na *'Beira'* na vile vile jamii mbalimbali za Matembele. Kwa maelezo zaidi na upatikanaji wa viazi vitamu lishe (OFSP) na matembele tutembelee katika kituo chetu au wasiliana na:cbonaventure@echonet.org

---

Mambo muhimu ya kuwazia katika kanda msimu huu:

Ugonjwa wa Mahindi- "*Maize Leathal Necrosis Disease*" (MLND) katika Afrika Mashariki

Kwa wakulima wa Afrika Mashariki katika kipindi hiki cha mvua ni vema wakafahamu kwamba kuna ugonjwa wa mahindi unaojulikana kitaalamu "Maize Leathal Necrosis Disease" (MLND). Ugonjwa huu hutokea wakati virusi vya aina mbili yaani Maize Chlorotic Motile Virus" na "Sugarcane Mosaic Virus" (SCMV) vinapoathiri mmea wa mhindi kwa pamoja. Hakuna dalili za ugonjwa huu ambazo hujitokeza pale kinaposhambulua kirusi cha aina moja tu. Ugonjwa huu ummetokea katika maeneo mbali mabali ya Arusha ikiwa ni pamoja na eneo letu la kituo cha ECHO katika kanda ya Afrika Mashariki. Unaweza kujifunza jinsi ya kukabiliana na ugonjwa huu kwa kusoma zaidi HAPA.

Mashamba huambukizwa na wadudu ambao kuhamisha ugonjwa huo. Kwa vile virusi hawa huathiri pia na nafaka, haishauriwi mazao kuliwa na binadamu wala na mifugo. Mimea iliyoambukizwa inapaswa kuondolewa kutoka shamba mara moja.

Utabiri wa hali ya hewa:Elinino mwaka 2014

Utabiri wa hivi karibuni unabashiri kuwepo kwa mvua kubwa za Elinino kama zilivyowahi kutokea katika miaka ya 1997 hadi 1998.Mabadiliko ya hali ya hewa yameathiri mamilioni ya watu na kuwa na madhara makubwa yatokanayo na mafuriko, ukame, na mabadiliko ya joto.

Kama tabiri hizi zitakuwa sahihi , kanda ya Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na nchi za Uganda , Kenya , Burundi , Rwanda, na Tanzania zinaweza kuwa na mvua zaidi , wakati maeneo ya kusini ikiwa ni pamoja na nchi za Msumbiji na Zimbabwe zinaweza kuwa na kiasi kidogo cha mvua kuliko kawaida. Kujifunza zaidi kuhusu utabiri wa Elinino bonyeza HAPA.

ECHO East Africa News

Edited By: Erwin Kinsey and Brian Lawrence